


What is primary prevention? Je, Uzuiaji wa msingi ni nini?

Kwa pamoja tunapaswa kukomesha dhuluma dhidi ya wanawake kabla ifanyike.

Hii ndio kazi ya uzuiaji wa msingi na ndio kazi ya White Ribbon inapozingatia.

Hata hivyo tunaweza kuainisha uzuiaji na kukabiliana na dhuluma kwa njia mbalimbali, kwa mfano:



Katika maelezo haya, tunachunguza aina tofauti za kuzuia dhuluma zilizoonyeshwa katika picha iliyo hapa juu.


Uzuiaji wa Msingi

Hatua ya uzuiaji wa msingi ya kukomesha dhuluma za wanaume dhidi ya wanawake hutokelezwa kabla ya dhuluma kufanyika na inalenga kukomesha uwezekano wa wanaume na wavulana kuwadhulumu wanawake na wasichana. Hatua hii ya uzuiaji hufanya hivi kwa kushughulikia chanzo cha sababu za dhuluma. Kampeni ya White Ribbon na mipango ya husika hulenga uzuiaji wa msingi.

Mifano ya uzuiaji wa msingi ni pamoja na:

- Maelezo ya umma na kuhamasisha watu katika vyombo vya habari, maeneo ya kazi na jamii
- Mipango ya elimu shuleni
- Mipango katika maeneo ya kazi
- Sera ya serikali ya kuanzisha mipangilio na viwango vya kuzuia dhuluma dhidi ya wanawake na kukuza usawa wa kijinsia.

Uzuiaji wa msingi unalenga jamii kwa ujumla.



Uzuiaji wa Pili

Uzuiaji wa pili unalenga kuzuia dhuluma dhidi ya kuendelea au kuongezeka. Uzuiaji wa pili hufanikiwa wakati dhuluma zinaepukwa au kukomeshwa: waathiriwa hawaathiriki tena (k.m. kuacha uhusiano wenye dhuluma) au wahusika kuacha kuwa wakatili.

Mifano ya uzuiaji wa pili ni pamoja na:

- Ziara za nyumbani kutoka kwa wafanyakazi wa ustawi wa jamii kwa akina mama waliojifungua walio katika hatari ya kudhulumiwa
- Mipango ya mabadiliko ya kitabia kwa wanaume walio na matatizo ya kudhibiti hasira.

Uzuiaji wa pili unalenga watu na vikundi vilivyo katika hatari ya kuathirika au watekeleza dhuluma. Watu walioponea dhuluma na wahusika hufaidika pia na uzuiaji wa pili.



Uzuiaji wa Tatu

Mikakati ya uzuiaji wa tatu hutekelezwa baada ya dhuluma kufanyika. Uzuiaji wa tatu hulenga kupunguza athari ya mzozo, kurejesha afya na usalama na kuzuia dhuluma dhidi ya kufanyika tena.

Mifano ya uzuiaji wa tatu ni pamoja na:

- Makazi ya dharura
- Ushauri na utetezi
- Mfumo wa haki kwa wahusika

Kazi hii inaweza kusaidia uzuiaji wa msingi na wa pili kwa kupunguza ufanyaji makosa na uonevu zaidi. Uzuiaji wa tatu huchangia pia uzuiaji kwa njia isio ya moja kwa moja kwa kusaidia kubadilisha fikra za jamii kuhusu dhuluma dhidi ya wanawake. Kwa mfano, wakati wanajamii wanashuhudia mfumo wa sheria ukiadhibu mizozo ya kijamii, kuna uwezekano mkubwa zaidi kuwa wanaweza kuwaunga mkono waathirika na makabiliano ya kisheria dhidi ya dhuluma.

Uzuiaji wa tatu unalenga waathirika na wahusika wa dhuluma.

